Hadithi Ya Mvuvi Masikini

Swahili Text

Hadithi, Hadithi.

Hapo zamani za kale aliishi mvuvi masikini ambaye kwa jina aliitwa Majuto. Majuto aliishi kwenye kijiji kidogo pembeni mwa ziwa dogo pamoja na familia yake. Kwa miaka mingi sana watu wa kijiji hicho walikuwa wakiishi wakitegemea ziwa hilo kwaajili ya samaki na maji kwa matumizi yao yote. Waliweza kukamata samaki wakuwatosha wao na pia wachache ambao waliweza kuuza kwenye vijiji vya jirani ili kujipatia mahitaji mengine.

Kila asubuhi Majuto aliamka mapema na kutayarisha ngalawa na ndoano yake na kwenda kuvua samaki ili aweze kuipatia familia yake chakula. Ngalawa yake ilikuwa ni kubwa na imara sana yenye uwezo wa kwenda umbali mrefu juu ya maji bila tatizo lolote. Lakini Majuto alikuwa sio mvuvi mzuri kwa kuwa aliogopa sana maji na hakujua kuogelea. Kila siku aliwaza sana kabla ya kupanda ngalawa yake na alifikiria itakuwaje kama ikizama au ikipata shida ya aina yeyote na akadumbukia kwenye maji. Ni kwa sababu tu alikuwa hana njia nyingine ya kujipatia yeye na familia yake chakula ndio alilazimika kwenda na kuvua samaki. Rafiki zake Majuto walijaribu kumfundisha jinsi ya kuogelea lakini kila alivyoweka tu mguu wa kwanza ndani ya maji alihisi kama vile anazama na aliamua kukimbia. Kweli tatizo lake la kuogopa maji lilikuwa ni kubwa na ni sugu.

Kila asubuhui Majuto alienda na ngalawa yake kuvua samaki lakini aliishia tu kutega ndoano yake kandokando mwa ziwa ambapo hapakuwepo na samaki wengi. Alifanikiwa kumkamata samaki mmoja mmoja tu na ndoano yake na mwisho wa siku alikuwa amekata jumla ya samaki watatu au wanne tu wadogo. Hili jambo liliendelea kila siku, aliondoka asubuhi na mapema na alirudi jioni na samaki wachache sana. Uwoga wake wa maji ulimsababisha asiweze kufanikiwa zaidi kama walivyo fanya wavuvi wengine ambao waliweza kwenda umbali mrefu zaidi na kukamata samaki wengi zaidi waliokuwa wakubwa.

Masikini Majuto siku zilivyopita uwonga wake haukupungua na alibakia kuwaza sana jinsi atakavyofanya ili aweze kupata samaki wengi zaidi. “Jamani jamani, nitafanya nini masikini mimi. Mbona wenzangu wanafanikiwa na mimi nashindwa”, alilalamika Majuto. Aliwaza sana mpaka ghalfa wazo lilimjia – “nitaenda kumuomba mchawi anisaidie na kuniondolea shida zangu zote”, alisema Majuto. Pamoja na kuwa alishasikia kwa wazee wa kijijini na pia kwa watu wengi kuwa mchawi huyo aliyekuwa akiishi milimani sio mtu mzuri, Majuto hakufikiri mara mbili. “Hii ndio nafasi yangu kubwa ya kuweza kubadilisha maisha yangu kabisa. Hao wanaosema kuwa hili sio jambo zuri hawapendi kuniona nimefanikiwa”, alisema Majuto.

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

Siku ikawadia na Majuto alifungasha virago vyake, aliiaga familia yake na kubeba zawadi ambazo alikuwa amemtayarishia mchawi. Bila kugeuka aliondoka upesi na kuelekea juu milimani alipokuwa akiishi huyo mchawi. Safari ilikuwa ni ndefu lakini Majuto alikuwa akitembea upesi sana. Alivuka mito, mabonde na misitu minene ambamo walikuwa wakiishi wanyama wengi wakali. Baada ya kutembea kwa muda mrefu Majuto alijikuta akipita kwenye uwanja mkubwa na kwa ghafla alitokea ndege mkubwa sana angani. Alikuwa na rangi ya zambarau na njano na mkia mrefu wa kuvutia. Majuto alishtuka sana alivyomuona huyo ndege kwa kuwa hakuwahi tena kuona ndege mkubwa hivyo aliyeruka angani. Alisimama mdomo wake ukiwa wazi kwa mshangao. Ndege huyo alitua chini ardhini na alizidi kumsogelea Majuto. Jasho jembamba lilimtoka Majuto na hakujua cha kufanya na alibaki amesimama tu bila kusema neno lolote. Ndege alisimama na kumuangalia Majuto machoni kisha akasema kwa sauti nzito, “Mtaka vyote hukosa vyote”. Kisha ndege aligeuka na kuruka angani na kupotea juu ya mawingu. Majuto hakuamini alichokiona na kusikia na alijihisi anaota. Alijaribu kutafakari lakini alikosa jibu na akaamua aendelee na safari yake ya kwenda kwa mchawi.

Baada ya kutembea kwa muda mrefu Majuto hatimaye alifika kwenye nyumba aliyoishi mchawi. Ilikuwa ni nyumba kubwa nyeupe iliyovutia sana. Mawe meupe yaliyo ng’aa yalikuwa yamepangwa vizuri kuelekea hadi mlangoni. Majuto alikuwa anauoga lakini alijikaza na akagonga mlango. ”Nani wewe?”, alisikia sauti ikitoka ndani ya nyumba. ”Ni mimi Majuto mvuvi masikini. Nimekuja kuomba msaada wako”. Mlango ulifunguliwa na hapo alikuwa amesimama mzee mmoja mfupi mwenye mvi nyingi. Alionekana ni mtu wa kawaida tu tofauti kabisa na hadithi zote alizokuwa amezisikia Majuto huko kijijini kwake. Majuto aliwaza kuwa labda amekosea nyumba na huyu sio yule mchawi ambaye watu walikuwa wakimsema. Ikabidi Majuto amulize ”je, wewe ndio mchawi?”. ”Ha ha ha” alicheka mzee, ”ndivyo watu wanapenda kuniita hivyo. Karibu sana ndani”.

Majtuo aliingia na kukaa chini kwenye mkeka. ”Ninaweza kukusaidiaje?” aliuliza mchawi. ”Nimefunga safari kutoka mbali kuja huku ili niombe msaada wako”, alisema Majuto. ”Mimi ni mvuvi lakini ninaogopa sana maji na hivyo inanizuiya kuweza kwenda mbali na ngalawa yangu ili nikatege ndoano yangu na kukamata samaki. Kila ninavyowaza jinsi ya kufanya nashindwa na ninabakia tu kando kando mwa ziwa ambapo samaki ni wachache na pia ni wadogo. Ninakuomba sana unisaidie kuondoa uwoga wangu wa maji ili niweze kujifunza kuogelea na kupata uhodari wa kwenda mbali zaidi na ngalawa yangu.” ”Lo, nimekuelewa”, alisema mchawi. ”Tatizo lako ni dogo sana. Subiri hapa nitakuletea dawa itakayo kusaidia”. Mchawi aliamka na kwenda uwani. Baada ya muda si mrefu alirudi huku ameshika chungu kidogo chenye kilichofanana na maziwa. Alimpa Majuto kile chungu na kumwambia anywe.

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

Majuto alifanya hivyo. Baada tu ya kumaliza alisikia tumbo lake lina nguruma na mwili wote ulisisimka. Alianza kujisikia wa tofauti kama vile amekuwa mwepesi zaidi. Mchawi akamwambia Majuto, " Hii dawa imekufanya uwe mwepesi na kuanzia leo utaweza kuogelea bila ya kuzama". Majuto alifurahi sana na kumshukuru mchawi kwa msaada wake. Kuonyesha shukurani yake Majuto aliitoa zawadi yake aliyomletea na kumpa.

Wakati wa kuagana ulipofika Majuto alikuwa tayari kuondoka. "Asante sana mzee, sasa mimi nitarudi kjijini kuendelea na maisha yangu", alisema Majuto. "Ngoja kidogo." Alisema mchawi. "Kwani wewe usingependa nikuwezeshe pia kukamata samaki wengi zaidi? Kwanini nisikupe kifaa ambacho kitakuwezesha kukamata samaki wengi sana?" Majuto hakuamini alichosikia. "Mzee, yaani kuna kifaa ambacho kitaniwezesha kukamata samaki wengi zaidi?", alisema Majuto. "Ndio, nitakupa lakini itabidi ukubaliane na masharti yangu kwanza", alisema mchawi. "Niambie tu na mimi nitayatekeleza", alisema Majuto.

Mchawi aliondoka tena kuelekea uwani na kurudi na nyavu kubwa. Majuto hakuelewa ni nini kile alichokuwa amekishika mchawi kwa kuwa hakuwahi kuona nyavu maishani mwake. Siku zote yeye na wavuvi wenzake walikuwa wakitumia ndoano tu kuvulia samaki na hawakujua nyavu ni nini. Mchawi akasema, "Hii ni nyavu. Iweke ndani ya maji kila jioni, utakapo rudi jioni utakuta samaki wengi sana wamenasa kwenye matundu. Kazi yako itakuwa ni kuwaokota tu na kuwaweka ndani ya ngalawa yako." Majuto hakuamini masikio yake. "Kweli hii ni siku ya furaha sana maishani mwangu. Lakini kwanini unataka kunifanyia haya yote?" aliuliza Majuto. Mchawi alimjibu, "Hapo zamani niliwakosea watu wengi na nilifanya mambo mengi mabaya. Ndio maana ilinibidi nikimbilie na kuishi mwenyewe huku milimani. Lakini nimefikiria sana mambo niliyoyafanya na nimeyajutia ndio maana ninataka kuwasaidia watu. Sitakuomba mengi, lakini kila utakapoenda ziwani kuvua samaki ninataka uchukue nusu ya samaki wote uliowashika na kuwapa masikini na wazee wasiojiweza. Ukishindwa kuyatekeleza haya basi na wewe pia hautafanikiwa" Majuto haikumbidi hata kufikiria sana na alijibu, "Mimi pia ninapenda sana kwasaidia watu lakini tu sikuwa na uwezo. Sasa umeniwezesha na mimi pia nitawasaidia watu wengine zaidi ya hata uliyoniambia."

Kwa maneno hayo waliagana, na Majuto alibeba nyavu aliyopewa na mchawi na kuelekea tena kurudi nyumbani. Alikuwa na furaha kubwa sana na alikimbia upesi sana hadi kufika nyumbani kwake. Hakuwaza hata kusimama na kusalimia familia yake na kuwaambia kuwa amerudi, alikimbia moja kwa moja hadi kwenye ziwa na kujitupa kwenye maji. Na kweli mchawi alivyokuwa amesema Majuto hakuzama. Alibaki tu juu ya maji akielea. Majuto alishangilia sana na kwenda kuwatangazia rafiki zake

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

wote yaliyomkuta. Nao pia wakabaki kufurahi naye kwasababu Majuto alikuwa ni rafiki yao wa siku nyingi.

Jioni ilivyofika na wavuvi wengine wakiwa wanarudi majumbani mwao, Majuto ndio alianza kuandaa ngalawa yake. Alizipandisha nyavu alizopewa na mchawi huku akitabasamu. ”Leo ndio maisha yangu yanabadilika, shida zangu zote ninaziacha nyumba”, alisema Majuto. Alipanda ndani ya ngalawa yake na kuondoka kuelekea ziwani. Giza lilikuwa linaingia taratibu lakini Majuto hakuwa na wasiwasi kabisa na alizidi kwenda mbali. Baada ya kusogea kwa muda, miti iliyokuwa ikiota kando mwa ziwa ilizidi kuonekana midogo. Nyumba za kijiji nazo zilizidi kuonekana ndogo alivyozidi kwenda mbali. Alikuwa amebakia mwenyewe tu kwenye ziwa, watu wote walikuwa wamesharudi majumbani kwao na kupumzika kwa siku hiyo.

Ghafla Majuto alisikia mlio wa ndege ikitoka angani. Aligeuka kwa haraka na kuangalia juu. Ilikuwa ni kama ndoto imejirudia, yule ndege mkubwa aliyejitokeza kwenye safari yake ya kwenda kwa mchawi alikuwa amerudi. Majuto aliogopa sana kwa kuwa alijua yuko peke yake na hakuna mtu wa kumpa msaada wowote. Ndege alizunguka ngalawa mara mbili halafu akatua juu ya yake. Walibaki wanaangaliana tu kwa muda mrefu kisha ndege akafungua mdomo akasema, ”Mtaka vyote hukosa vyote”. Kisha ndege aligeuka na kuruka angani na kupotea juu ya mawingu. Majuto alibaki tena kuwaza sana nini maana ya hayo maneno. Kwanini ndege amwambie kuwa akitaka vyote atakosa vyote? ”Mimi sina tamaa”. Alisema Majuto. ”Kwa hivyo ninajua kuwa sitaweza kupata shida ambazo ameniambia ndege”.

Basi Majuto aliendelea hadi sehemu ambapo wavuvi wengine walisema kuwa kuna samaki wengi. Alishusha nyavu ndani ya maji kama mchawi alivyokuwa amemwelekeza. Nyavu zilikuwa ni nyepesi na alifanikiwa kuziweka ndani ya maji bila ya kupoteza muda. Alibaki kusubiri hapo hapo mpaka giza likaingia bila ya kitu chochote kutokea. ”Mchawi aliniambia kuwa nitakamata samaki wengi sana lakini Mbona hakuna dalili yeyote hapa?”, alisema Majuto. Masaa yalizidi kusogea na giza lilitanda lakini Majuto alivumilia huku akisubiri ishara yoyote kuwa kuna samaki amekamatwa lakini hapakutokea kitu. Usingizi ulianza kumshika Majuto na baada ya muda si mrefu alisinzia.

Mjuto hakuamka mpaka pale ambapo jua linaanza kuchomoza upande wa pili mwa ziwa. ”Kweli nimehangaika bure”, alisema Majuto. ”Nimekesha usiku mzima na hakuna samaki hata mmoja.” Kwa huzuni kubwa alianza kuzivuta nyavu iliazirudishe kwenye ngalawa. ”Mbona nyavu zimekuwa nzito sana?”, alijiuliza. ”Au ni kwa kuwa zimeloa?”. Alizidi kuvuta kwa nguvu zake zote ndio nyavu zikaanza

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

kupanda taratibu. Majuto aliangalia kwa makini zaidi na alishtuka kuona kuna samaki mmoja amekwama kwenye nyavu. Alizidi kuvuta nyavu na mara akaonekana samaki mwengine mkubwa zaidi naye amekwama kwenye nyavu. Majuto alizidi kufurahi na kuvuta nyavu kwa nguvu zaidi. Kila akizivuta na samaki wengi wakubwa walikuwa wakizidi kupanda juu. Majuto alishangilia kwa sauti kubwa na kupiga kelele kwa furaha. Alimalizia kupandisha nyavu na kuanza kuhesabu samaki. Walikuwa ni wakubwa na wengi sana mpaka alishindwa kuhesabu wote. Majuto hakupoteza muda, aligeuza ngalawa yake na kuelekea kurudi kijijini.

Majuto alipokaribia kufika aliiona familia yake na rafiki zake wengi wakimsubiri kando ya ziwa. Aliwapungia mkono kuwaonyesha kuwa kila kitu kilikuwa ni salama. Kweli ilikuwa ni siku ya furaha kubwa kwa Majuto na familia yake yote. Majuto aliwapa rafiki zake wote samaki. Pia aliwapa masikini na wazee wasiojiweza kama mchawi alivyokuwa amemwelekeza Majuto. Watu wote siku hiyo walifurahi kwa pamoja. Pamoja na kwamba alikuwa amewapatia ndugu na marafiki samaki wengi bado alikuwa amebakiwa na wengine wengi. Majuto alipeleka samaki waliobaki sokoni na kuwauza kwa bei nzuri sana na kupata fedha nyingi.

Maisha ya Majuto na familia yake yalibadilika. Kila jioni Majuto alienda ziwani na kutega nyavu zake na kurudi asubuhi na samaki wengi sana. Nusu ya samaki wote aliokamata aliwapa masikini na wazee, baada ya hapo alienda sokoni na kuuza samaki waliobaki kwa faida kubwa. Haikuchukua muda mrefu na Majuto alipata uwezo wa kujenga nyumba kubwa ya kifahari yenye vyumba vingi. Nje alipanda bustani kubwa ya maua na kufuga wanyama na ndege wengi wa kifahari kutoka nchi za mbali. Pia alikuwa na wafanyakazi wengi wa ndani ambao walifanya kazi zote za ndani ili mke wake na watoto wake wasipate taabu yeyote. Majuto alianza kujivuna na mali zake na hatimaye aliamua kuwa kazi ya kwenda ziwani kila siku kukamata samaki haimfai yeye, aliamua kuajiri vijana wachache wakufanya hiyo kazi. Kweli maisha yake na familia yake yalikuwa ni mazuri.

Usiku mmoja Majuto alikuwa amelala kitandani ndoto ikamjia. Aliota kuwa yuko kwenye chumba kidogo kisichokuwa na madirisha wala milango. Alijaribu sana kutoka lakini alishindwa. Ghalfla yule ndege mkubwa ambaye Majuto alishakutana naye mara mbili alitokea. Ndege alibaki tu anamwangalia Majuto kisha akasema, “Mtaka vyote hukosa vyote.” Kisha ndege akapotea. Majuto aliamka kwa mshituko mkubwa lakini alivyojua kuwa ni ndoto tu alitulia kidogo. “Lah, kumbe ni ndoto tu.” Alisema Majuto. Alitafakari ndoto yake kwa muda mfupi lakini hakuona kama vile ni jambo lolote la kushitua na akarudi kulala. Kesho yake maisha yaliendelea kama kawaida.

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

Lakini haikuwa ni rahisi kutunza vyote hivi mwenyewe na kisha ilimbidi Majuto kuajiri wafanyakazi wengi wa kutunza nyumba na mali zake zote. Pia Majuto alianza kuwa na wasiwasi juu ya usalama wake. Alifikiria kuwa kama haya yote yametokana na yeye kuwa na nyavu, je nyavu hii ikipotea au ikiibiwa, itakuwaje? Basi aliamua kuajiri walinzi wengi pia wakumlinda yeye na mali zake zote. Walinzi wengine aliwaajiri kwa kulinda nyavu tu.

Pamoja na mali zake zote Majuto alizojikusanyia, bado alikuwa anataka mengine mengi. Alitaka awe na nyumba kubwa zaidi na ya kifahari zaidi. Alipenda awe na wanyama wengi wa kutoka nchi za mbali zaidi na wafanyakazi wengi zaidi. Pia alitaka aweze kusafiri nchi za mbali na aweze kurudi na zawadi nyingi kwa ajili ya familia yake.

Mali za majuto zilivyozidi kuwa nyingi na taabu na mawazo yalizidi kuwa mengi. Gharama za kulipa wanfayakazi wake wote zilizidi na baadala ya kufurahia maisha yake mazuri alianza kuwaza sana. “Haya yote nitaweza kuyatekeleza kweli iwapo nusu ya kipato changu chote nitaendelea kuwapa masikini?” Alisema Majuto. “Hata hivyo nimeshawasaidia vya kutosha. Kuanzia sasa itabidi nianze kujifikiria mwenyewe na matakwa yangu.” Kuanzia siku hiyo Majuto aliamua kuwapa masikini robo tu ya mapato yake. Majuto alifikiria, “Mchawi kweli aliniambia niwape masikini nusu ya mapato yangu yote, lakini kwa sasa ninadhani nimeshawasadia vya kutosha. Kwani mchawi atajuaje kuwa siwapi masikini nusu ya mapato yangu.” Kufanya hivi kulimwezesha kuendeleza maisha yake ya kifahari. Alijenga nyumba kubwa zaidi na kuajiri wafanyakazi wengi zaidi. Pia alisafiri mbali zaidi na kurudi na zawadi nyingi zaidi kwa familia yake.

Lakini kama ilivyokuwa mara ya kwanza, gharama za kutunza mali zake zote zilizidi kuwa kubwa. Hatimaye Majuto aliamua kuwapa masikini robo ya mapato yake haitawezekana tena. Aliamua kuwa kuanzia sasa yeye mwenyewe ndio atakayefaidika na kazi yake. Aliacha kabisa kuwasaidia masikini na wazee na pia tabia yake ilibadilika. Majuto hakuwa tena mtu mwenye roho nzuri kama watu walivyokuwa wakimfahamu. Alibadilika na kuwa mtu mwenye hasira za haraka na alibaki kugombana sana na watu, hata rafiki zake wa karibu. Mtu yeyote mwenye shida akimfuata Majuto alikataa kabisa kumpa msaada hata kama alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Mara nyingine alitumia hata walinzi wake kuwafukuza watu hao wenye shida.

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

Siku moja Majuto alikuwa akitembea kwenye bustani yake alitokea bibi kizee mmoja na kumwambia Majuto, “Tafadhali sana naomba unisaidie nimepata shida. Nyumba yangu ambapo nilikuwa nikiishi na mtoto wangu mmoja na mjukuu wangu imeshika moto na kuteketea kabisa. Sina pakuishi wala chakula. Ninakuomba unisaidie kwa lile utakalo weza.” Majuto alicheka kwa sauti kubwa, “ Ha ha ha, wewe bibi kizee unatembelea magongo hata nikikusaidia wewe utaweza kunisaidia nini.” Hapo sauti ya Majuto ilibadilika na aliongea kwa ukali sana, “Ondoka upesi sana hapa na usirudi tena! Nyie watu mnakuwa hamna shukurani kabisa. Muda wote huu nimewasidia lakini mpaka leo mnaendelea tu kuja kwangu kuomba misaada. Ondoka haraka na usirudi tena.” Masikini bibi kizee alianza kuondoka kwa kunyong’onyea.

Ambacho Majuto alikuwa hajaona ni kuwa juu ya mti mkubwa uliokuwa kando yake yule ndege mkubwa alikuwa amekaa na anaona yote yaliyokuwa yakitokea. Alitoa kelele kubwa kwa hasira “Ng’waaaa!” Kisha ndege huyo aliruka na kutua mbele ya Majuto na kuongea. “Majuto, nimekupa kila ulichotaka na kukuongezea mengine mengi. Sharti lilikuwa ni moja tu. Wape masikini na wasiojiweza nusu ya mapato yako. Lakini hili umekuwa na tamaa na kusahau watu wengine.” Kwa maneno hayo ndege aligeuka na alibakia hapo amesimama mchawi. Kumbe siku zote hizo Majuto hakujua kuwa yule ndege ndio mchawi. Alikuwa amejigeuza ili aweze kumkumbusha majukumu yake kama tajiri. Lakini Majuto alizidiwa na tamaa na kuamua kutojali watu wenye shida. “Mtaka vyote hupoteza vyote. Na wewe leo umepoteza vyote. Hili liwe onyo kwako. ” Alisema mchawi.

Upepo mkali ulianza kuvuma kwa ngurumo mkubwa na vumbi lilitimka. Ardhi yote ilitetemeka na miti ilitikisika. Majuto alifunga macho na kuziba masikio kwa uwoga. Baada ya muda mfupi upepo uliisha na kila kitu kilitulia. Majuto alifungua macho yake taratibu na kuangalia huku na kule. Alidhani kuwa amehamishwa kwenda sehemu nyingine. Nyumba yake na bustani na mali zake zote zilikuwa zimetoweka. Mchawi naye pia alikuwa ametoweka. Kilikuwa kimebakia tu kibanda alichokuwa akiishi zamani. Alianguka chini na kutoa kilio kikubwa.

Majuto aliamka tena na kutembea taratibu kwa kujivuta mpaka kwenye banda lake na kuchungulia ndani. Aliona familia yake bado ilikuwepo na wote walikuwa wazima. Aliweza kusikia amani kidogo kuwa hao bado walikuwa ni wazima. Majuto aliingia ndani ya banda na kutazama vizuri huku machozi bado yanamtoka. Alishtushwa kuona kuwa bado nyavu alizokuwa amepewa na mchawi zilikuwa zimelala kwenye mkeka.

Hadithi Ya Mvuvi Masikini

“Hili litakuwa ni fundisho kwangu.” Alisema Majuto. Pamoja na masikitiko yake yote Majuto alikuwa amejifunza kitu cha muhimu sana. Tamaa ya mali inakufanya usifikirie kuhusu shida za watu wengine. Inabidi kumsaidia mtu mwenye shida pale unapoweza bila kubagua. Kuanzia siku hiyo Majuto alianza kujenga maisha yake upya lakini alibaki kukumbuka maneno aliyokuwa akimkumbusha kila mara, “Mtaka vyote, hupoteza vyote.” Na mpaka leo hii Majuto anaishi maisha mazuri sana kando mwa ziwa na familia yake wakipendana na kusaidiana na watu wote wengine.